JARIDA KUHUSU |UTALII | UHIFADHI NA MASUALA MBALIMBALI

# TZ&BEYOND

APRIL-MAY 2023 | ISSUE NO 007

Multisectoral magazine



MCHANGO WA SEKTA BINAFSI KATIKA **HUDUMA** YA AFYA NCHINI

HUDUMA ZA KUSAFISHA **FIGO** ZARAHISISHWA ZAIDI TANZANIA

## BIMA YA AFYA
### KWA WOTE INAWEZEKANA

TSHS.25,000 KSHS.1,300 USHS 40,000
ISSN 2799-225X | LESENI 00000021
www.tz&beyond.co.tz




# BODI YA WAHARIRI

AFISA MTENDAJI MKUU
**Emmanuel J. Kakuyu**
Cell: 0622411148
ekakuyu@gmail.com

MHARIRI MTENDAJI
**Jimmy C. Kiango**
Cell: 0787 180 065
jimmy.kiango@tz&beyond.co.tz

MSANIFU KURASA
**Felix Jimmy**
Cell: 0763 520 319
felix.aloyce@tz&beyond.co.tz

MWANDISHI
**Hassan Daud**
Cell: 0692 695 889

MWENYEKITI/MLEZI
**Dk. Thomas Kashililah**
[fclpp, cipm,ChE, AFA]
Cell: 0754 997 645
namkonda@gmail.com

**TZ&BEYOND**
Mbezi Beach Park Building;
Off Bagamoyo Road
P.O. Box 79010, Postcode: 14121
Phone: +255 655 06 38 39
Dar Es Salaam , Tanzania

**MAUZO/MATANGAZO**
Sales Team,TZ&BEYOND
Cell: 0655063839
email: tz1andbeyond@gmail.com




www.tz&beyond.co.tz







08
Bima ya afya kwa wote ni muhimu na inawezekana



20
Serikali chini ya Rais Samia imedhamiria kuboresha sekta ya afya



45
Vision Plus kinara wa matibabuya macho Tanzania





22
Mchango wa sekta binafsi katika huduma ya afya nchini



40
Shree Hindumandal Hospitali yenye Miaka 104





28
Huduma za kusafisha figo zarahisishwa zaidi Tanzania





32
Hospitali ya TMJ kimbilio la wengi

# TZ&BEYOND




***Jarida hili linalowafikia watu wa rika na kada*** mbalimbali ndani na nje ya Tanzania limelenga kukupa maarifa ambayo huwezi kuyapata kwenye jarida lolote **Tanzania**.

**TZ&BEYOND** limejikita kwenye kuchambua masuala ya siasa, Bunge, Uchumi, Mazingira, Uhifadhi na Habari za kimataifa dhamira yake kuu ni kuwa darasa mikononi mwako.

***TUNA MWANZO, HATUNA MWISHO***

USIKOSE KUSOMA MAJARIDA YETU KUPITIA TOVUTI

www.tz&beyond.co.tz




## JICHO LA TZ&BEYOND



MHARIRI MTENDAJI: JIMMY C. KIANGO
JARIDA: TZ&BEYOND
COVER STORY: BIMA YA AFYA KWA KILA MTANZANIA INAWEZEKANA

# TUMSAIDIE RAIS DKT. SAMIA KUFANIKISHA NIA NJEMA YA BIMA YA AFYA KWA WOTE

Tangu uhuru, Serikali imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali ya kupambana na maadui wakuu watatu wa maendeleo ambao ni ujinga, maradhi na umaskini Katika kupambana na adui maradhi, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuandaa na kutekeleza Sera za ugharamiaji wa huduma za afya, kutoa huduma za afya bila malipo kwa wananchi zoezi lililofanyika mwaka 1961-1990, utaratibu wa uchangiaji wa huduma za afya na utaratibu wa msamaha kwa wananchi wasio na uwezo jukumu lililoanza kutekelezwa mwaka 1990 na utaratibu wa malipo kabla ya kuugua ambao unajulikana kama bima ya afya ambao sasa ndio unapigiwa chapuo.

Pamoja na jitihada hizo, bado kumekuwa na changamoto katika utekelezaji wa mifumo ya ugharamiaji huduma za afya kama ifuatavyo, utaratibu wa malipo ya papo kwa papo na utaratibu wa msamaha kusababisha baadhi ya wananchi kukosa huduma kutokana na kukosa fedha za kugharamia huduma za matibabu katika vituo vya kutolea huduma,

Idadi ndogo ya wananchi katika mfumo wa bima ya afya (asilimia 15.3 ya wananchi wote) kutokana na uhiari (NHIF;8%,CHF: 6%, NSSF-SHIB; 0.3% na bima binafsi: 1%).

Uhiari wa kujiunga na bima ya afya na hivyo kusababisha wananchi kujiunga wakiwa wagonjwa kinyume na kanuni za bima.

Sasa serikali imeandaa muswada wa Bima ya Afya kwa wote, chimbuko lake ni kutimiza wajibu wa Serikali wa kikatiba wa kuhakikisha wananchi wote wanapata huduma bora za afya bila vikwazo.

Uhalisia unaonyesha kuwa idadi kubwa ya wananchi (asilimia 85) hawana bima ya afya na hivyo kukosa uhakika wa kupata huduma za afya pindi wanapozihitaji.

Wizara imefanya tathmini mbili za uhai na uendelevu wa mifuko ya bima ya afya ili kubaini gharama za matibabu, kupitia Mshauri Elekezi wa kimataifa (Muhanna and CO . Ltd, Lebanon) ilifanya tathmini ya uendelevu wa Mifuko mwaka 2020.

Tathmini ya NHIF ilifanyika mwaka 2022 (Zamara Actuaries Adminstrators and Consultants Ltd, Kenya)

Aidha, kumekuwa na mapitio ya taarifa mbalimbali za tathmini zinazotolewa na mamlaka zenye dhamana ya kuandaa viashiria vya mwenendo wa uchumi.

i. Integrated Labor Survey
ii. Natinal Bureau of Statistics

Tathmini zote mbili za mwanzo zimeonesha kuwa uhimilivu wa mifuko unategemea idadi kubwa ya wanachama kujiunga na mfumo wa Bima. Uhiari wa kujiunga ni changamoto katika utekelezaji wa mfumo wa bima ya afya nchini, Wanachama na makundi yote walioingia kwa hiari wametumia huduma zaidi ya michango yao kwa wastani kati ya asilimia 212 kwa mwaka 2020 hadi asilimia 369 kwa mwaka 2021.

Kiwango cha uchangiaji cha asilimia 6 kwa watumishi wa umma na wafanyakazi wa sekta rasmi binafsi ni muhimu kuendelea,

Viwango vya uchangiaji vipangwe kwa kuzingatia hali halisi ya gharama za matibabu na uwezo wa wananchi kuchangia.

Wastani wa pato la mwezi ni shilingi 137,789 kwa ajira isiyo rasmi (NBS 2021/22)wastani wa pato kwa mwezi kwa wanaojishughulisha na kilimo ni shilingi 169,375 (ILS 2021)

Matumizi katika matibabu kwa mwananchi ni Tsh. 96,760 kwa mwaka (NHA, 2020); Matibabu kwa mnufaika wa NHIF ni Tsh.109,467 sawa na shilingi 412,947 kwa kaya kwa mwaka;

Matibabu ya Saratani ni Tsh. 45,691,980 kwa mwaka, usafisha damu (Dialysis) mgonjwa (mahudhurio 3) anatumia Tsh. 240,000 (kwa hudhurio), shilingi 2,880,000 (mwezi) sawa na shilingi 34,560,000 (mwaka); Upasuaji wa Moyo: Wastani wa shilingi Tsh. 2,991,635.36 kwa Mgonjwa kwa mwaka; Shinikizo la juu la damu ni Tsh. 279,000 kwa mwezi sawa na Tsh. 3,353,000 kwa mwaka Kisukari (wanaotumia dawa tu ni Tsh. 140,000 kwa mwezi na wanaotumia Sindano (Insulin Injection) ni Tsh. 190,000 kwa mwezi

Ukiangalie gharama zilizoanishwa hapo juu utagundua kuwa ni za juu na haziwezi kuhimilika kwa mtu wa kipato cha chini.

Hata hivyo yapo mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada ambayo ni kuwa na kitita cha mafao ya huduma muhimu ambacho kila Skimu ya Bima ya afya italazimika kukitoa na kitakuwa haki ya kila mwanachama; Kitita cha mafao cha huduma muhimu kitabeba huduma ya ada ya uandikishaji na kumuona Daktari, gharama za vipimo, dawa aina zote (NEMLIT), upasuaji mdogo na mkubwa, kulazwa, huduma ya afya ya kinywa na meno, matibabu ya macho, vifaa saidizi na huduma za mazoezi ya

Ili kufanikisha haya serikali imeahidi kuimarisha mifumo ya TEHAMA.

Kaya ya watu sita itaundwa na mwanachama mchangiaji, mwenza na wategemezi wasiozidi wanne (04)

Mifuko ya bima ya afya ya Umma na Kampuni binafsi za bima ya afya kzitapaswa kufanya tathmini ya uhai na uendelevu kila baada ya miaka mitatu (03);

Waziri mwenye dhamana ya masuala ya afya atakuwa na mamlaka ya kuboresha Mifuko ya bima ya afya ya Umma;

Mamlaka ya usimamizi na udhibiti wa bima nchini (TIRA) itapewa jukumu la kuimairisha usimamizi na udhibiti wa masuala ya bima ya afya.

Wananchi wasio na uwezo watawezeshwa kupata huduma za afya baada ya kutambuliwa na Mamlaka husika ambapo watagharamiwa upatikanaji wa huduma za afya na wizara ya fedha ndio itakuwa na jukumu la kutenga fedha.

Ili kulifanikisha hili, kuna haja ya watanzania wote kumsaidia Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.



# Bima ya afya kwa WOTE inawezekana

**Wataalamu wataja faida zake, kuisaidia Tanzania kupiga hatua za maendeleo**

07







# Bima ya afya *kwa* WOTE inawezekana

Oktoba 31, mwaka 2022 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan alitangaza matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika Oktoba 23, mwaka huohuo.

Katika matokeo hayo Rais Dk. Samia alibainisha kuwa idadi ya Watanzania ni 61,741,120. Aidha, kati ya watu hao 59,851,357 wapo Tanzanzia Bara na 1,889,773 wapo Tanzania Zanzibar.

Dk. Samia aliendelea kwa kusema kwamba wanawake wapo 31,687,990 sawa na asilimia 51 ya watu wote na wanaume ni 30,530,130 sawa na asilimia 49 ya watu.

Hata hivyo, wakati hali ikiwa hivyo, takwimu za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) zinabainisha kuwa ni asilimia 8 tu ya Watanzania ndiyo wanaotumia huduma ya bima ya afya ambapo wengi ni wafanyakazi. Hatua hiyo imekuwa ikisababisha mzigo mkubwa kwa mfuko huo na hata wakati mwingine kujiendesha kwa kusuasua.

Utafiti wa TWAWEZA wa mwaka 2017 ulipewa jina la Sauti za Wananchi Afya kwanza, ulibainisha kuwa kati ya Watanzania wanne basi ni mmoja tu mwenye bima ya afya.

Wakati hali ikiwa hivyo, Wizara ya Afya nchini inabainisha kuwa asilimia 99 ya watu wenye bima ya afya nchini, wamejiunga wakiwa wagonjwa huku wengine wakilazimika kuuza mali zao kuhudumia wagonjwa waliopo hospitalini kutokana na kukosa bima.

## MPANGO WA SERIKALI

Katika Bunge la lililoisha mwanzoni mwa mwaka huu jijini Dodoma Serikali kupitia Wizara ya afya ilipanga kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ambao ulikwama na matarajio ni kuuwasilisha kwenye Bunge linaloendelea sasa.

**Waziri Ummy amefafanua zaidi kuwa lengo la Serikali kufungamanisha bima ya afya na huduma zingine ni kutaka kuhakikisha wananchi wote wanakuwa na bima.**



# Bima ya afya *kwa* WOTE inawezekana

**Nitoe wito kwa Watanzania kuanza kudunduliza ili kuwa na gharama za matibabu kabla ya kuugua na hatutomuacha nyuma Mtanzania yeyote**

WAZIRI WA AFYA UMMY MWALIMU

Moja ya mambo muhimu yaliyomo katika muswada huo ni pamoja na kila Mtanzania kupatiwa huduma za afya hata kwa wale wasio na uwezo.

Sambamba na hilo, wizara imefafanua kuwa kwa upande wa wastaafu waliokuwa wakichangia bima ya afya binafsi, iwapo muswada huo utapita, watalazimika kujiunga na skimu ya bima ya afya ya umma ili kuwa na sifa ya uchangiaji wa miaka 15.

Kuwasilishwa bungeni kwa muswada huo itakuwa ni mara ya pili baada ya awali kuondolewa mwaka jana kutokana na kile kilichoelezwa kuwa, ni kukosekana kwa chanzo halisi cha mapato ya kuwezesha kutoa huduma hizo kwa wote.

"Kwa awamu hii ili kuwa na uendelevu wa mfuko tunachoangalia ni michango, kama vile ilivyo kwa mifuko ya hifadhi ya jamii ya NSSF, PSSSF na WCF, kwamba uwe walau umechangia kwa miaka 15.

"Tunataka walau awe amechangia kwa miaka 15 kwenye bima ya afya, wastaafu ndiyo wenye matumizi makubwa kutokana na kushambuliwa zaidi na magonjwa yasiyo ya kuambukiza," anasema Waziri Ummy.

Mwenyekiti wa kikosi kazi cha muswada huo wa Bima ya Afya kwa Wote, Bernard Konga anasema kuwa hata kama mtu amechangia miaka 15 kwenye bima za sekta binafsi, hataweza kunufaika na bima hizo baada ya kustaafu.

Konga ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) anafafanua kuwa mchangiaji huyo sasa atapaswa kuwa na michango isiyopungua miaka 15 katika skimu ya umma.

Waziri Ummy anasena kuwa: "Nitoe wito kwa Watanzania kuanza kudunduliza ili kuwa na gharama za matibabu kabla ya kuugua na hatutomuacha nyuma Mtanzania yeyote," anasema Ummy.

Waziri Ummy amefafanua zaidi kuwa lengo la Serikali kufungamanisha bima ya afya na huduma zingine ni kutaka kuhakikisha wananchi wote wanakuwa na bima.

Mtaalamu na mshauri wa masuala ya afya, Dk. Elisha Osati anasema Serikali inapaswa kuangalia ni namna gani itawahusisha wananchi wengi na mfumo wa Bima ya Afya kwa Wote akisisitiza kwamba wagonjwa wengi wasio na uwezo wa kulipia huduma za afya ni mzigo kwenye sekta ya afya.

Anasema bila kuwa na bima ya afya ni mzigo mzito kwa Mtanzania na Taifa kwa ujumla.

Akizungumza na TZ&BEYOND kuhusu faida na hasara za mpango huo Dkt. Elisha anasema kuwa faida za bima ya afya ni nyingi kuliko hasara.

"Bima ni kitendo cha kuchangia ukiwa bado hauumwi, kwa maana kwamba wazima wanachanga kwa ajili ya wale ambao wanaumwa au unajiwekea mazingira ya baadae pindi utakapoumwa.

"Hivyo, hii inakuondoa katika ule mfumo wa kutoa fedha zako mfukoni kwa ajili ya kujihudumia pale utakapokuwa unaumwa wewe pamoja na familia yako kinyume na utakavyokuwa na bima.





**Sasa hivi wenye bima wanakimbilia hospitali za binafsi kuliko za serikali kwa sababu ya ubora wa huduma**

RAIS WA TANZANIA HEALTH SUMMIT, DK. OMARY CHILO

"Kama unavyojua kwamba sisi Watanzania wengi ni watu wa kawaida kiuchumi ambapo pindi mtu unapougua hadi uje ujihudumie basi utatumia fedha nyingi hadi kupona tofauti na ukiwa na bima, kwani inakupa uhuru wa kutibiwa mahala popote nchini na kupatiwa huduma kulingana na kifurushi chako," anasema Dk. Osati.

Akizungumzia hasara za bima na ile ambayo itapatikana iwapo Serikali itapitisha mpango huu, mtaalamu huyo anasema kuwa hakuna hasara itakayopatikana zaidi ni manufaa ambayo watayapata Watanzania na taifa kwa ujumla kupitia mpango huo.

Anasema nchi inaweza kumudu kufanikisha mpango huo kutokana na kuwa na raslimali nyingi.

"Kwenye hili matarajio yetu ni kwamba Serikali itaweka fedha kwanza kabla ya watu kuanza kuchangia, hivyo kwenye hili tunaamini kuwa itaweza kugharamia kwanza.

"Sote tunafahamu kwamba vitu vyote ambavyo vinasababisha magonjwa mengi kutokea hasa haya yasiyo ya kuambukiza ni kunywa pombe kupita kiasi, sigara na vitu vyenye sukari, hivi vyote vinaweza kuchangia kiasi kidogo kwenye bima na kufanya mfuko kuwa na fedha za kutosha.

"Kwa hiyo tunao uwezo tukijipanga vizuri na hata watu binafsi tunatumia fedha nyingi kwenye harusi na mambo mengine ya kupita, tunaweza kutumia kiwango hicho kwa ajili ya kujiunga na bima na ikatumika kwa mwaka mzima, hivyo ninachoweza kusema hapa ni kwamba huo uwezo tunao kama taifa," anasema Dk. Osati.

### CHANGAMOTO ZA NHIF

Akizungumzia kuhusu changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikiukabili mfuko wa NHIF Dkt. Osati amesema kuwa zinasababishwa na kuzidiwa kwa mfuko. "Changamoto za NHIF zinajulikana bayana kabisa, nafikiri haya mabadiliko yote ambayo tunayaona ni sababu mfuko ni mdogo na huu ndiyo ukweli, hivyo unakutaka kwamba asilimia 8 hawa wanaochangia ndiyo wanahudumia watu wengine hawa zaidi ya milioni 50.

"Hivyo, kwa namna yoyote ile lazima utaona kama mfuko ni mdogo kwani kumbuka kuwa wenye mfuko nao wanajitahidi kuhakikisha kwamba haufi, hivyo unakutaka kwamba kazi ni kubwa, mbaya watu wengi zaidi ya asilimia 90 ya wanaojiunga na bima wanakuwa tayari wanaumwa, lakini kwa sasa utaimarika kwa kuwa watakaochangia watakuwa ni wengi iwapo mpango huu utafanikiwa," anasema Dk. Osati.

### NAFASI YA TANZANIA KIMATAIFA

Anasema kukamilika kwa mpango huo kutaenda kuiunganisha Tanzania kwenye orodha ya nchi nyingine ambazo tayari zinatumia mfumo huo.

"Nchi nyingi za Scandnavia, Rwanda, Ghana, Norway, Finland, Japan na nyinginezo zinatoa huduma ya afya kwa watu wake wote, hivyo huu ni mpango ambao umekuja wakati muafaka," anasema Dk. Osati na kuongeza kuwa sekta ya afya nchini bado inakabiliwa na changamoto nyingi na kwamba zitaendelea kutatuliwa kidogo kidogo.

Kwa upande wake Rais wa Tanzania Health Summit, Dk. Omary Chilo anasema kuwa ubora wa huduma za afya lazima uendane na uchangiaji.

"Sasa hivi wenye bima wanakimbilia hospitali za binafsi kuliko za serikali kwa sababu ya ubora wa huduma," anasema Dk. Chilo.

Pia anasisitiza kuwa kinga ikizingatiwa idadi ya watu wanaohitaji huduma ya matibabu itapungua. Sheria ya bima ya afya inayopendekezwa itaitambua NHIF kama Mfuko wa Bima ya Afya wa Umma utakaohudumia watumishi wa umma na wananchi wengine watakaochagua kujiunga na mfuko huo







### UDHIBITI

Bernard Konga ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa NHIF akizungumzia kuhusu mamlaka ya udhibiti wa bima ya afya anasema kuwa jukumu hilo litatekelezwa na TIRA.

"Katika hili nimesema kwamba tumeimarisha usimamizi na udhibiti wa masuala ya bima ya afya, jukumu litakalotekelezwa na Mamlaka ya Bima Tanzania (TIRA), pia tumezingatia dhana ya ufungamanishaji wa huduma wenye lengo la kutaka kila mtanzania anafikiwa na mpango huu," anasema Konga.

Aidha, akifafanua kuhusu hoja hiyo, Waziri Ummy amesema mapendekezo ya awali ya huduma zilizofungamanishwa na upatikanaji wa bima zilikuwa tisa.

"Baada ya majadiliano, tuliona kuna baadhi ya huduma zinapaswa kuondolewa ambazo ni utambulisho wa mlipa kodi, usajili wa laini za simu, hati za kusafiria, utoaji wa kitambulisho cha Taifa na usajili wa wanafunzi wa kidato cha tano na sita," amesema Ummy.









### SERIKALI ILIVYOJIPANGA

Akizungumzia maandalizi ya serikali kuwahudumia wananchi wote, Konga anasema kuwa kuna ongezeko la vituo vya kutolea huduma za afya kutoka 8,449 hadi kufikia vituo 10,067.

Amesema Serikali inatoa Sh. bilioni 20 kila mwezi kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa dawa, hadi kufikia Desemba 2022 upatikanaji wake ulikuwa kwa asilimia 67 kutoka asilimia 62 Agosti, mwaka jana.

"Serikali imenunua na kusimika vifaa vya kisasa vya uchunguzi na matibabu ikiwemo X-Ray (95) CT Scan (30) na MRI (4) katika vituo vya kutolea huduma. Pia wizara inaendelea kutekeleza mkakati wa kuongeza rasilimali watu katika sekta na mwaka 2020/2021 watumishi 3,347 na mwaka 2021/2022, iliajiri watumishi 9,262. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, wizara imetenga Sh bilioni 8 kwa ajili ya ufadhili wa mafunzo ya ubingwa na ubobezi,"alisema.

Upande wake Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Profesa Abel Makubi anasema kuwa ili kuiwezesha TIRA ifanye kazi zake kwa ufanisi, serikali itaiongezea mamlaka hiyo wataalam.

Kamishna wa Bima Tanzania, Dk. Baghayo Saqware amesema mambo yote ya msingi yamezingatiwa kwenye muswada wa bima ya afya ikiwemo vitita vinavyopendekezwa.

### WANANCHI WASUBIRI KWA HAMU

Daniel Humble Mkazi wa Dar es Salaam anasema kuwa iwapo mpango huo utafanikiwa na Watanzania wakajiunga basi vikwazo vinavyojitokeza vinapaswa kuondolewa mara moja.

"Pia ni vema kama tukafungamanishe na huduma ya simu, kwa mujibu wa takwimu za Serikali kuna akaunti za kifedha(mobile money) wastani wa milioni 35, kila mmoja akichangia kiwango cha chini Sh. 500 na kuendelea kwa mwezi ambao taifa litaweza kukusanya fedha nyingi kwa mwaka naamini tutafanikiwa katika mpango huu," anasema Humble.

Upande wake, Machiya Shija anasema kuwa mpango huo ni vema gharama zake zikapungua ili kuondoa mzigo kwa wafanyakazi.

"Bima kwa wote ipunguzwe gharama kwa sababu hili litakuja kugeuka kuwa mzigo kwa mfanyakazi wa Serikali kwa kulazimika kukata bima kwa ajili ya familia yake kila mwaka, walau gharama ziwe rafiki," anasema Shija.

Steven Mgisha anasema kuwa: "Hii bima ya wote ni jambo zuri ila chonde chonde isiwe kama ICHF iliyoboreshwa kama nchi tumepata hasara sana maana mgonjwa anakata bima ya 30,000 hapo hapo na anapatiwa matibabu zaidi ya 30,000 hata mwaka hajamaliza na wenzake hawajatibiwa yaani hili lilikuwa bomu kwa vituo.

"Bima ya afya ni muhimu sana kwa kila nchi, kikubwa ni elimu itolewe kwa kila mwanchi aelewe ni kwanamna gani hii bima itamsaidia pindi anapopata matatizo ya kiafya," amesema Mgisha.

Laurent Abel anasema kuwa yeye kuhusu bima ya afya kwa wote haelewi chochote na kwamba ni vema elimu zaidi ikatolewa kwa wananchi ili kazi iwe nyepesi.

**Tumeimarisha usimamizi na udhibiti wa masuala ya bima ya afya, jukumu litakalotekelezwa na Mamlaka ya Bima Tanzania (TIRA), pia tumezingatia dhana ya ufungamanishaji wa huduma wenye lengo la kutaka kila mtanzania anafikiwa na mpango huu,**





## Muhimbili Mloganzila, ni moja ya hospitali inayotoa huduma ya upandikizaji wa figo




# MLOGANZILA



## 01

### Bernard Konga

MKURUGEZI MKUU NHIF

"Serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan imedhamiria kuboresha sekta ya afya kwa kutoamuacha nyuma Mtanzania kwa kuhakikisha kuwa anapata huduma ya afya popote alipo kwa kutumia kadi ya bima ya afya ya NHIF.



## 02

### Prof.Abel Makubi

KATIBU MKUU WIZARA YA AFYA

"ili kuiwezesha TIRA ifanye kazi zake kwa ufanisi, serikali itaiongezea mamlaka hiyo wataalam.





## 03

### Dk. Baghayo Saqware

KAMISHNA WA BIMA TANZANIA

"Mambo yote ya msingi yamezingatiwa kwenye muswada wa bima ya afya ikiwemo vitita vinavyopendekezwa



## 04

### Dk. Elisha Osati

MTAALAMU NA MSHAURI WA MASUALA YA AFYA

"Bima, kwani inakupa uhuru wa kutibiwa mahala popote nchini na kupatiwa huduma kulingana na kifurushi chako,



# MCHANGO WA SEKTA BINAFSI KATIKA HUDUMA YA AFYA NCHINI

**Jitihada za serikali zimekuwa zikiungwa mkono pakubwa na sekta binafsi, ambayo hakuna shaka yoyote wana mchango mkubwa katika mapinduzi ya utoaji wa huduma za afya nchini.**




MCHANGO WA

# SEKTA BINAFSI

KATIKA HUDUMA YA AFYA NCHINI

**Tunafanya kazi na mashirika ya kimataifa kama vile DANIDA na USAID ambao wamekuwa wakitusaidia kwa upande wa msaada wa kitaalamu**

WAKATI 'Tanzania' inapata uhuru wake Desemba 9,1961 idadi ya watu ilikadiriwa kuwa 12,313,469, na katika kipindi hiki huduma za afya zilikuwa mbovu na zisizoridhisha.

Hali ilikuwa hivyo kwa sababu hakukuwa na hospitali za kutosha, hakukuwa na vituo vya afya vya kutosha na hata zahanati zilikuwa chache.

Kibaya zaidi huduma za afya zilikuwa zikitolewa na serikali tu, hakuna mtu au taasisi binafsi ukiondoa zile za dini zilizoruhusiwa kuendesha shughuli ya utoaji wa huduma za afya.

Pamoja na ufinyu wa huduma, lakini pia zilizokuwepo zilitolewa kwa matabaka, ipo jamii hasa iliyowagusa wakoloni wenyewe, hii ilipewa huduma nzuri na jamii ya watu weusi wengi ilijikuta ikiangukia kwenye huduma duni hali iliyowalazimu wengi wa watu hao kukimbilia kwenye miti shamba.

Sasa ni wastani wa miaka 63 ya Uhuru, idadi ya watu imeongezeka na kufikia 61,741,120, idadi hiyo ni kwa mujibu wa Sensa ya watu na makazi iliyofanyika mwaka 2022.

Oktoba 31,2022 Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alitangaza matokeo ya Sensa hiyo na kubainisha kuwa idadi ya Watanzania ni 61,741,120 na kati ya watu hao 59,851,357 wapo Tanzanzia Bara na 1,889,773 wapo Tanzania Zanzibar. Wanawake wapo 31,687,990 sawa na asilimia 51 ya watu wote na wanaume ni 30,530,130 sawa na asilimia 49 ya watu.

Ukweli ni kwamba ongezeko hili la watu bado linatajwa kutoendana na uhalisia ulivyo kwenye utoaji wa huduma za afya nchini, eneo hili linakabiliwa na changamoto lukuki zikiwemo za uhaba wa vitanda vya wagonjwa, ukosefu wa dawa, uhaba wa wataalamu na upungufu wa vituo vya afya.

Imeelezwa kuwa ingawa sasa ni afadhali tofauti na ilivyokuwa huko nyuma, lakini ukweli ni kwamba kwenye hospitali za umma bado hali si ya kuridhisha.

**"Tumekuwa tukifanya kazi na serikali kwa karibu sana, mawasiliano yamekuwa mazuri na tunaendelea kuboresha huduma kila siku,**

Madhila hayo na mengine mengi yanaisababisha serikali kupoteza fedha nyingi kutokana na kugharamia matibabu ya baadhi ya wananchi wake nje. Hali ilikuwa mbaya zaidi miaka ya nyuma ambapo serikali ilikuwa ikitumia fedha nyingi kupeleka wagonjwa Ulaya na Marekani kusaka tiba bora.

Ahueni ilikuja kupatikana mara baada ya aliyekuwa Naibu Waziri wa Afya Tatu Mussa Ntimizi ambaye alikuwa Mbunge wa Igalula, Uyui mkoani Tabora kuongoza mazungumzo ya mageuzi ya kuwapeleka wagonjwa India badala ya Ulaya ambako gharama zilikuwa juu zaidi.

Ntimizi akiwa Naibu Waziri wa Afya, chini ya Waziri Dkt. Aron Chiduo katika Serikali ya Awamu ya Tatu iliyoongozwa na Marehemu Rais Benjamin Mkapa, aliisaidia nchi yetu kukubali kuwa India ilikuwa imepiga hatua kubwa katika sayansi ya tiba na gharama za matibabu zilikuwa chini kuliko Ujerumani au Ulaya yote, uamuzi huo ulilisaidia Taifa kuokoa mamilioni ya fedha za kigeni.

Ukubwa wa gharama za matibabu nje ya nchi umekuwa ukisukuma serikali kufanya jitihada mbalimbali za kuhakikisha kunakuwa na maboresho na mabadiliko makubwa katika kutoa huduma za afya nchini.

Katika kudhihirisha hilo Rais Dkt. Samia aliwahi kusema kuwa tumepata mafanikio makubwa

Tangu sekta binafsi kuruhusiwa kuendesha biashara ya kutoa huduma za afya 1996, kumekuwa na mageuzi na mabadiliko makubwa kwenye sekta hiyo.







Tunatoa huduma za ubora wa hali ya juu kabisa, ieleweke kuwa sisi sekta binafsi ndio tumekuwa wa kwanza kuleta vifaa vikubwa vya matibabu nchini, mashine ya CT Scan

kwenye sekta ya afya kwa kujenga vituo vya kutolea huduma za afya 1,887 (zikiwemo zahanati 1,198, vituo vya afya 487, hospitali za wilaya 99, Hospitali za Rufaa za Mikoa 10 na Hospitali za Rufaa za Kanda tatu).

Alisema katika kipindi chake cha uongozi ataimarisha upatikanaji wa huduma za afya kwa kuendelea kujenga miundombinu, kuongeza watumishi, vifaa tiba, dawa na vitendanishi na kuongeza juhudi za kupunguza vifo vya wajawazito na watoto.

Jitihada hizo za serikali zimekuwa zikiungwa mkono pakubwa na sekta binafsi, ambayo hakuna shaka yoyote wana mchango mkubwa katika mapinduzi ya utoaji wa huduma za afya nchini.

Tangu sekta binafsi kuruhusiwa kuendesha biashara ya kutoa huduma za afya 1996, kumekuwa na mageuzi na mabadiliko makubwa kwenye sekta hiyo.

Ujio wa sekta binafsi kwenye eneo la utoaji wa huduma za afya, ulisaidia nchi kuanza kuingiza mashine na vifaa vikubwa vya matibabu kama alivyoainisha Mwenyekiti wa Chama cha Watoa Huduma za Afya Binafsi Nchini APHFTA, Dkt Egina Francis Makwabe.

Katika mahojiano yake na jarida hili, Dkt. Makwabe ambaye ni Daktari bingwa wa magonjwa ya ndani ya mwili ukiwemo ugonjwa wa figo, alisema tangu wameanza kazi wana miaka zaidi ya 20, na mafaniko makubwa ambayo sisi tunajivunia ni kukubalika na kuaminika na jamii.

"Tunatoa huduma za ubora wa hali ya juu kabisa, ieleweke kuwa sisi sekta binafsi ndio tumekuwa wa kwanza kuleta vifaa vikubwa vya matibabu nchini, mashine ya CT Scan ya kwanza kabisa katika nchi hii imeletwa na Hospitali ya Kairuki Mikocheni, kwahiyo tumekuwa ni watu ambao tunavumbua teknolojia mpya zaidi, huduma za kusafisha damu na huduma za upasuaji kwa njia ya matobo zote zimefanyika nchini kwa mara ya kwanza kwenye hospitali binafsi na hii yote ni kwasababu tumeshikamana kama kitu kimoja.

"Tumekuwa tukifanya kazi na serikali kwa karibu sana, mawasiliano syamekuwa mazuri na tunaendelea kuboresha huduma kila siku, na tunafanya kazi na mashirika ya kimataifa kama vile DANIDA na USAID ambao wamekuwa wakitusaidia kwa upande wa msaada wa kitaalamu na ufadhili wa pesa kidogo, yote hiyo ni katika kuboresha huduma katika vituo vyetu."

Dkt. Makwabe alisema kuwa katika kuhakikisha wanasaidiana na serikali katika kutoa huduma bora za afya, tayari wao kupitia wanachama wao wameweza kujenga zaidi ya Hospitali 1600 nchi nzima, Zahanati na vituo vya afya nchi nzima zaidi ya 1000, maabara zinazojisimamia zaidi ya 1000, famasi zaidi ya 1000 na maduka ya dawa baridi zaidi ya 18,000 nchi nzima.

"Hii ni hatua kubwa kwetu na tunajivunia katika hili, maana ukiangalia hali ilivyokuwa kabla ya sekta ya afya kuruhusiwa kutoa huduma na sasa, kuna mabadiliko.

" Hata baadhi ya huduma za afya za kibingwa kwa sasa zinatolewa nchini, hii inasaidia kuiondolea mzigo serikali katika kuwahudumia baadhi ya wananchi wake nje ya nchi."






JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA (TMDA)

TMDA
Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

KUHUSU TMDA

*Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ambayo ilikuwa ikijulikana kama Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ni taasisi ya Serikali iliyo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambayo ina jukumu la kulinda afya ya jamii kwa kudhibiti usalama, ubora na ufanisi wa dawa, bidhaa za tumbaku, chanjo, vifaa tiba na vitendanishi.*

*Iliyokuwa TFDA ilibadilishwa jina na kuwa TMDA mnamo tarehe 1 Julai, 2019 kufuatia marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura 219 kupitia Sheria ya Fedha, Na. 8 ya mwaka 2019 ambayo mbali na kubadili jina la Sheria hiyo kuwa Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura 219, pia ilihamisha majukumu ya kudhibiti ubora na usalama wa chakula na vipodozi kwenda katika Sheria ya Viwango, Sura 130.*

**DIRA** | Kuwa Mamlaka inayoongoza katika kudhibiti usalama, ubora na ufanisi wa dawa, chanjo, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa nyingine zinazohusiana na afya kwa wote

**DHIMA** | Kulinda afya ya jamii kwa kuhakikisha usalama, ubora na ufanisi wa dawa, chanjo, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa nyingine zinazohusiana na afya.

MAJUKUMU

1 Kusajili na kutoa vibali vya majengo ya kutengeneza na kuuza dawa, chanjo, bidhaa za tumbaku, vifaa tiba na vitendanishi

2 Kukagua maeneo ya kutengeneza na kuuza dawa, chanjo, bidhaa za tumbaku, vifaa tiba na vitendanishi

3 Kukagua shehena za bidhaa za dawa, chanjo tumbaku, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya forodha na kwenye maghala ya kuhifadhia bidhaa hizi

4 Kutoa vibali vya kuingizia na kusafirisha nje ya nchi bidhaa za dawa, chanjo, tumbaku, vifaa tiba na vitendanishi

5 Kusajili bidhaa za dawa, chanjo, tumbaku, vifaa tiba na vitendanishi kabla ya kuruhusiwa kuuzwa katika soko la Tanzania

6 Kudhibiti majaribio ya dawa, chanjo, bidhaa za tumbaku na vifaa tiba na kufuatilia madhara yatokanayo na matumizi ya bidhaa hizi

7 Kudhibiti matangazo ya dawa, chanjo, bidhaa za tumbaku, vifaa tiba na vitendanishi

8 Kutoa elimu kwa umma

Imetolewa na:
Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA),
S.L.P 77150, Dar es Salaam au
S.L.P 1253 Dodoma
Simu: +255 222 450512/450751/452108
Simu ya Bure: 0800110084
Nukushi: +255 222 450793
Barua Pepe: info@tmda.go.tz Tovuti: www.tmda.go.tz

0800110084 @tmda_tanzania @tmda tanzania www.tmda.go.tz "TMDA Hulinda Afya ya Jamii"



# HUDUMA ZA KUSAFISHA FIGO

## ZARAHISISHWA ZAIDI TANZANIA

**MTANDAO wa Huduma za Afya Afrika maarufu kama Afrika Healthcare Network Tanzania Ltd (AHN) sasa umerahisha kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa huduma za usafishaji wa figo (dialysis) nchini.**



**Mtandao huo hadi sasa unao vituo 16 vya kutoa huduma ya kusafisha figo nchini Tanzania.**



Huduma za kusafisha figo

MTANDAO wa Huduma za Afya Afrika maarufu kama Afrika Healthcare Network Tanzania Ltd (AHN) sasa umerahisha kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa huduma za usafishaji wa figo (dialysis) nchini.

Mbali ya kurahisisha upatikanaji wake, lakini pia inatoa huduma hiyo kwa kwa gharama nafuu sanjari na kuisogeza huduma hiyo na huduma za kibingwa na kibobezi karibu na wananchi.

Mtandao huo hadi sasa unao vituo 16 vya kutoa huduma ya kusafisha figo nchini Tanzania.

Akizungumza na jarida hili, Mkurugenzi wa Tiba kutoka AHN, Dk Egina Makwabe, alisema mtandao huo ambao upo kwenye nchi mbalimbali za Kusini mwa Jangwa la Sahara, umekuwa ukifanya kazi ya kutoa huduma za afya na hasa afya ya magonjwa ya ndani ukiwemo usafishaji wa figo.

Alisema wamekuwa wakifanya kazi hiyo kwa kushirikiana na mashirika bora ya afya Tanzania na Afrika kwa ujumla, ambapo wamefanikiwa kuweka vituo 16 vya kusafisha figo.

"Tumekuwa tukifanya hivyo tangu mwaka 2018 kwa nafuu na pia bima ya afya inatumika, tunafanya kazi vizuri na hospitali 16 nchini, kikubwa kinachofanywa na mtandao wetu ni kuendesha vituo hivyo, lakini pia tunajenga na kuleta mashine za kisasa, wataalamu na wafanyakazi na kuanza kutoa huduma," alisema Dk. Makwabe.

Alizitaja baadhi ya hospitali wanazoshirikiana nazo katika mikoa mbalimbali nchini kuwa ni Hindumandal, CCBRT, Cardinal Rugambwa Ukonga,jijini Dar es Salaam, Serian Arusha, Saint Francis Ifakara Morogoro, Saint Joseph Peraminho Ruvuma, Nkinga Mission Hopital , Saint Joseph Sengerema na Saint Joseph Kilimanjaro.

Dk. Makwabe alisema wamekuwa wakitoa huduma hiyo kwa njia ya kushirikiana na hospitali hizo, ambapo wao wamekuwa wakipeleka vifaa na wataalamu huku washirika wao wakitoa maeneo.

Alisema fedha inayopatikana imekuwa ikitumika kwa shughuli za uendeshaji wa shughuli hiyo, ikiwa ni pamoja na kuwalipa wataalamu na ukarabati wa mashine zinazo haribika.

Akijibu swali la kutokuwepo kwa Hospitali inayosimamiwa na taasisi za Kiislamu, alisema: Bahati mbaya mpaka sasa hatujapata Hospitali ambayo inasimamiwa na taasisi yeyote ya kiislamu, lakini kuna hospitali mpya inayosimamiwa na taasisi ya kiislamu ipo Tabata, bado haijafunguliwa, hii itakuwa chini ya BAKWATA kwa asilimia 100, tayari tumeanza kufanya mazungumzo nao na ikiwa tayari tutashirikiana nao katika kutoa huduma hiyo," alisisitiza

Mtandao huo wa kwanza kuanzishwa Kusini mwa Jangwa la Sahara umekuwa ukitoa huduma za afya kwa kutoa huduma za afya.

AHN ilianzishwa nchini Tanzania kama Africa Healthcare Network Tanzania Limited Machi 3, 2017.

**Dk. Makwabe alisema wamekuwa wakitoa huduma hiyo kwa njia ya kushirikiana na hospitali hizo, ambapo wao wamekuwa wakipeleka vifaa na wataalamu huku washirika wao wakitoa maeneo.**







MMILIKI WA HOSPITALI YA TMJ, DKT. TYAVAL MOHAMED HUSSEIN JAFFERJI (KULIA), AKIWA NA MHARIRI MTENDAJI WA JARIDA LA TZ&BEYOND, JIMMY KIANGO



TMJ HOSPITAL LTD

# HOSPITALI YA TMJ KIMBILIO LA WENGI

**Bima ya Afya kwa wote ni muhimu sana, uwepo wake utalisaidia taifa kumiliki wananchi wenye uhakika wa huduma ya afya.**

MMILIKI WA HOSPITALI YA TMJ, DKT. TYAVAL MOHAMED HUSSEIN JAFFERJI

SUALA la afya ya mtu linapewa kipaumbele cha hali ya juu kwenye nchi mbalimbali duaniani. Moja ya maeneo yanayopewa nafasi kubwa hata kwenye bajeti za nchi ni eneo la afya.

Kwa Tanzania hali iko hivyo pia, na ndio maana kwa miaka mingi serikali imekuwa ikipambana kuhakikisha inatunisha mfuko wa wizara ya Afya ili iwe rahisi kuboresha miundo mbinu, wataalam na hata vifaa tiba.

Mathalani katika mwaka wa fedha wa 2022/23 wizara hiyo ilipata mgawo wa bajeti wa shilingi 1.109 trilioni, kiasi hiki cha fedha ni kikubwa kutofautisha na mgao uliotolewa kwenye wizara nyingine nyingi.

Wakati serikali ikipambana katika kuhakikisha huduma ya afya inapatikana katika viwango vya juu nchini, sekta binafsi nayo imekuwa mstari wa mbele kusaidiana na serikali katika kufanikisha hilo.

Hospitali ya TMJ ni miongoni mwa Hospitali binafsi ambazo zimekuwa kimbilio la wengi kutokana na uwezo wake wa kutoa huduma bora na kwa gharama nafuu.

Ukweli wa hilo umedhibitishwa na mmiliki wa hospitali hiyo Dkt. Tyaval Mohamed Hussein Jafferji katika mazungumzo yake na jarida hili.

Katika mahojiano hayo pamoja na mambo mengine, Dkt. TMJ alieleza historia yake pamoja na Hospitali hiyo ambayo alisema ilianza kwenye chumba kimoja.Ufuatao ni mtiririko mzima wa mahojiano hayo:-

**TZ&BEYOND:** Ni ipi historia ya TMJ?

**DKT. TMJ:** Jina langu kamili ni Tyavali Mohamed Hussein Jafferji maarufu kama TMJ, nilizaliwa Zanzibar, nikakulia na kusoma huko, wazazi wangu walikuwa wakiishi Pemba na baada ya kufanya mitihani yangu ya elimu ya juu  nilikwenda India kusomea udaktari, mwaka 1972 nilimaliza nikarudi Tanzania na kuanza kazi Hospitali ya Muhimbili.

**TMJ HOSPITAL LTD**

## Mafanikio yetu makubwa ni kuwepo kwa maabara kubwa yenye wataalmu wazuri kabisa ambayo mpaka sasa haihudumii Tanzania tu bali hata wenzetu kutoka nchi jirani za Kenya na Uganda wanaleta sampuli zao kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

**TZ&BEYOND:** Ni ipi historia ya **TMJ?** **DKT. TMJ:** Jina langu kamili ni Tyavali Mohamed Hussein Jafferji maarufu kama TMJ, nilizaliwa Zanzibar, nikakulia na kusoma huko, wazazi wangu walikuwa wakiishi Pemba na baada ya kufanya mitihani yangu ya elimu ya juu nilikwenda India kusomea udaktari, mwaka 1972 nilimaliza nikarudi Tanzania na kuanza kazi Hospitali ya Muhimbili.
Pamoja na kusomea udaktari India, lakini nakiri kuwa Muhimbili ilikuwa ni sehemu ambayo nimejfunza zaidi udaktari chini ya Maprofesa wangu wawili; Prof. Unoli na Prof. Kimati, hawa watu nawashukuru sana, walinifundisha udaktari kwa ufasaha.

Nilianza kazi yangu kwenye wodi ya watoto 'Pediatric Ward' nikiwa na mwalimu wangu Prof. Kimati. Ushirikiano wangu na Dkt. Kimati ulitusukuma kujenga wodi ya makuti hapohapo Muhimbili. Wodi ile ilisaidia kuokoa maisha ya watoto, jukumu letu kubwa lilikuwa ni kuwatengenezea watoto mchanganyiko wa vyakula vya lishe, tulifanikiwa kwakweli. Mwaka 1978 nilianzisha zahanati ndogo tu ya Burhan maarufu kama Burhan Charitable Dispensary. Niliiendesha zahanati hiyo kwa takriban miaka 10 nikiwa katika chumba kimoja na wengi walikuwa wakiitambua kama hospitali ndogo. Mwaka 1998 wakati tayari serikali imeruhusu kuanzishwa kwa hospitali binafsi, nilipata fursa ya kufungua 'Clinic' yangu mjini na hapo tayari nilikuwa na uzoefu wa kuendesha hospitali na nilianza na vitanda vinne. Kabla ya hapo hopsitali pekee zilizoruhusiwa kuanzishwa zilikuwa ni zile zilizomilikiwa na mashirika ya dini tu na sio watu binafsi.

**Hospitali ya TMJ ni miongoni mwa Hospitali binafsi ambazo zimekuwa kimbilio la wengi kutokana na uwezo wake wa kutoa huduma bora na kwa gharama nafuu.**

**TZ&BEYOND:** Wewe uliwezaje kutoa huduma za afya binafsi wakati haikuwa ikiruhusiwa?
**DKT. TMJ:** Haikuwa hospitali, ilikuwa ni zahanati tu.
**TZ&BEYOND:** Uliwezaje kuanzisha Hospitali yako?

**DKT.TMJ:** Mwaka 1990 nilimpa matibabu ya awali ya moyo mama mmoja hivi, kisha nikamtafutia hospitali nzuri Ulaya kwa matibabu zaidi.
Kwa sababu ya kufanikiwa kumsaidia yule mama, mume wake alinipa zawadi ya hili eneo ambalo hospitali ya TMJ ipo leo. Mwanzo nilikataa, nilikataa kwa sababu niliamini nimetekeleza wajibu wangu, yule bwana alisisitiza, nilikubali, yeye mwenyewe alibadili jina la kiwanja kutoka kwenye jina lake kuja kwenye jina langu.



**Nilianza kazi yangu kwenye wodi ya watoto 'Pediatric Ward' nikiwa na mwalimu wangu Prof. Kimati.**

DKT. TYAVAL MOHAMED HUSSEIN JAFFERJI




Wakati huo eneo hili lilikuwa ni kama bonde la mpunga, nikaingia gharama ya kupabadilisha kwa kujaza udongo.
Baadae nikapata mkopo wa benki kutoka kwa yule jamaa, ndio nikaanza ujenzi.
Nakumbuka baba yangu aliniuliza hela za kufanya haya yote nimezitoa wapi, niliwajibu kirahisi tu nimekopa, na ni kweli nilikopa benki. Hapo ndipo hospitali ya TMJ ambacho ni kifupi cha jina langu ilipoanza.

**TZ&BEYOND:** Hospitali ya TMJ ina wafanyakazi wangapi?
**DKT. TMJ:** Hospitali yetu imeajiri wafanyakazi 180 ambao ni wa muda wote na wengine 15 ambao ni madaktari wa muda.

**TZ&BEYOND:** Vifaa tiba na wataalamu ni moja ya changamoto kubwa katika hospitali nyingi, hali ikoje TMJ?
**DKT. TMJ:** Kwa upande wetu hatuna changamoto yoyote ya vifaa, tumekuwa tukijitahidi kuagiza vifaa vya kisasa mara kwa mara na tunashukuru serikali imekuwa ikitusaidia kwenye eneo hilo maana imeruhusu kuagiza vifaa vya kitabibu. Lakini pia benki zetu nchini zimekuwa ni msaada mkubwa sana kwetu, tumekuwa tukipata mikopo kwa haraka ndani ya muda mfupi, tunafanya nao kazi vizuri sana. Lakini hili pia limekuwa jepesi hata kwa wao kufanya kazi na sisi kutokana na rekodi yetu nzuri ya kurejesha fedha. Tuna vifaa tiba vyote muhimu hapa na wagonjwa wanatibiwa bila wasiwasi na kwa wakati na tunaamini hospitali hii ni kimbilio la wengi maana sisi tunajitahidi kumtibu mgonjwa ili aondoke hapa akiwa na afya njema, furaha yetu ni kuona mgonjwa anatoka geti la hospitali akiwa tofauti na alivyokuja.

**TZ&BEYOND:** TMJ ni moja ya hospitali kongwe nchini, ina matawi mengine nje ya Dar es Salaam?
**DKT. TMJ:** Kwa nje ya Dar es Salaam hatuna tawi lolote, lakini kwa hapa Dar es Salaam tuna tawi moja maeneo ya Chang'ombe.

**TZ&BEYOND:** Ni ipi nguvu yenu kama Hospitali?
**TMJ:** Nguvu yetu kubwa ni rasilimali watu,vifaa na huduma bora na rahisi, watu wanafanya kazi kwa uadilifu wa hali ya juu.
Tuna madaktari bingwa kabisa wanaotoa huduma za kisasa na kwa wakati. Pia kuwapo kwa wafanyakazi wachapakazi na waaminifu kunatufanya kujiamini zaidi.
Uongozi wa hospitali unawajali wafanyakazi wake, tunaboresha maisha yao kwa mfano kuwajengea makazi ya kudumu na kuwasaidia kwenye suala la elimu kwa watoto wao na hata wao wenyewe, mimi najali sana elimu, elimu ndio kipaumbele changu cha kwanza. Kwenye suala la gharama hapa ndipo tumeweka nguvu zaidi, sisi tunatibu kwa gharama nafuu ukilinganisha na wengine.

**Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ni muhimu kwa maendeleo ya sekta ya afya**



**Sekta binafsi inapaswa kupewa kipaumbele kwa vivutio vya kodi na punguzo ili wawekezaji wengi waweze kuleta utaalamu wa matibabu unaohitajika kwa wananchi wetu.**

MMILIKI WA HOSPITALI YA TMJ, DKT. TYAVAL MOHAMED HUSSEIN JAFFERJI




# Teknolojia ya kisasa kutumika katika matibabu



Hatutolei macho pesa bali tunajali sana utoaji wa huduma bora na si vinginevyo. Na hii ni kwasababu maisha ya binadamu ni ya muhimu sana kuliko kitu kingine. Huwa hatukatai kutibu mgonjwa kisa hawezi kulipia gharama za matibabu, utu ni muhimu.

**TZ&BEYOND:** Ushirikiano wenu na serikali ukoje?
**DKT. TMJ:** Tunashirikiana vizuri sana na serikali, zipo changamoto chache, lakini tunapata msaada mkubwa katika kuendesha shughuli zetu za kila siku.
Na tunalifanikisha hili kwa sababu tumekuwa tukifuata taratibu zote zilizowekwa, ambapo kama watoa huduma za afya nchini hatujawahi kuwa na tatizo na serikali na hii ni pamoja na kulipa kodi zote kwa wakati.

**TZ&BEYOND:** Serikali inapambania suala la Bima ya Afya kwa wote, je, hili litafanikiwa na lina tija?
**TMJ:** Bima ya Afya kwa wote ni muhimu sana, uwepo wake utalisaidia taifa kumiliki wananchi wenye uhakika wa huduma ya afya. Binafsi naamini litafanikiwa ingawa linahitaji umakini wa hali ya juu, maana ni lazima iangaliwe fedha za wasiokuwa na uwezo zitatoka wapi. Lakini pia ni rahisi kupata fedha hizo, serikali inaweza kuongeza kodi kwenye sigara au pombe, zikaelekezwa kwenye kuhudumia eneo la afya.

**TZ&BEYOND:** Ni yapi mafanikio ya hospitali ya TMJ?
**DKT. TMJ:** Mafanikio yetu makubwa ni kuwepo kwa maabara kubwa yenye wataalmu wazuri kabisa ambayo mpaka sasa haihudumii Tanzania tu bali hata wenzetu kutoka nchi jirani za Kenya na Uganda wanaleta sampuli zao kwa ajili ya uchunguzi zaidi. Tumepata kutambuliwa kitaifa na kimataifa na wadau mbalimbali kama watoa huduma bora. Mbali na hilo la maabara lakini pia serikali kututambua kama walipa kodi bora nayo ni suala la kujivunia. Mwaka 2007 tulitambuliwa kama walipa kodi bora nchini na kwakweli tumefanikiwa kupewa tuzo nyingine nyingi kwa miaka tofauti ambazo ni matunda ya utendaji wetu kazi kwa kuwahudumia watu bila kikomo na uaminifu mkubwa bila kusahau uwazi.

Na kingine ni kwamba mafanikio yetu makubwa ni pale tunapowatibu wagonjwa na kuwaona wakitoka hapa hospitali wakiwa wamepona, huwa tunafarijika sana.

**TZ&BEYOND:** Ushiriki wenu kwenye shughuli za kijamii ukoje?
**DKT. TMJ:** Tunafanya kazi na Lottery Club pia Lions Club na nyinginezo, tunasaidia watoto kwenye masuala ya afya, tunachimba visima kwenye shule kwa ajili ya kuwasaidia watoto maji ya kunywa. Na kwakua elimu ni kipambele changu cha kwanza, nimesaidia watoto wengi kielimu, na yote hii ni kwasababu nimeuishi umasikini hivyo ninajua umuhimu wa elimu.

**TZ&BEYOND:** Ni changamoto zipi mnakutana nazo katika utoaji wa huduma na ushauri wako ni upi kwa serikali na wadau wengine wa afya?
**DKT.TMJ:** Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ni muhimu kwa maendeleo ya sekta ya afya nchini Tanzania na viongozi wa serikali hawapaswi kuwaangalia wawekezaji binafsi kama adui zao, badala yake wanapaswa kujua sisi ni washirika wa maendeleo. Nashauri kusiwe na ucheleweshwaji wa vibali vya uendeshaji wa hospitali kwa sekta binafsi, tukiwa na hospitali nyingi zaidi upatikanaji wa huduma utakuwa ni wa urahisi na haraka. Sekta binafsi inapaswa kupewa kipaumbele kwa vivutio vya kodi na punguzo ili wawekezaji wengi waweze kuleta utaalamu wa matibabu unaohitajika kwa wananchi wetu.

Kulingana na Shirika la Afya Duniani (WHO), mfumo wa afya umeandaliwa vyema ambapo wahusika wa umma na binafsi kwa pamoja wanatekeleza utimilifu wa huduma ya afya kwa wote.

Tunapaswa kujenga maelewano kuhusu njia na mikakati bora zaidi ya kushirikisha sekta binafsi katika utoaji wa huduma za afya.
Nikimnukuu Peter Salama, "Huduma ya Afya kwa wote haiwezi kufikiwa bila sekta binafsi. Ni muhimu kuweka upya ushiriki wa sekta ya umma na binafsi kama ubia katika afya kwa matokeo ya pamoja ." Nikiangazia uzembe wa kimatibabu kuwa suala muhimu, napendekeza wakuu wa hospitali wachukue hatua zote zinazohitajika ili kuepuka uzembe wa kimatibabu. Usalama wa wagonjwa wakati wa matibabu hospitalini unapaswa kupewa umuhimu mkubwa.

Mamlaka za hospitali zinapaswa kuhakikisha nidhamu, nidhamu ni jambo la msingi kwa watoa huduma wa vitengo vyote. Hospitali zina wajibu wa kudumisha viwango vya maadili katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya na katika mawasiliano yote na wagonjwa na ndugu zao wa karibu. Uhamasishaji wa wafanyikazi katika suala hili unapaswa kufanywa na kila hospitali.

Ushauri wangu kwa wote.. Vituo vya afya vya serikali na binafsi viwawezeshe wataalamu katika utoaji wa huduma, kufanya kazi kwa uwazi, uendelevu na kwa ufanisi pamoja na uaminifu, ili kufikia malengo ya pamoja katika njia mpya ya kufanya biashara. Vilevile, tunahitaji kuwa na mikutano kati ya Serikali na Sekta Binafsi ili kuweza kutoa mawazo na mapendekezo yetu ambayo yataisaidia serikali kuepukana na changamoto zilizopo katika sekta ya afya nchini.

Mazungumzo ya mara kwa mara yataleta uelewa wa mausala muhimu na kuweka maridhiano ambayo lengo lake ni kujenga na sio kubomoa na hasa ni kuunga mkono juhudi za maendeleo ya nchi kwa ujumla wake kwa kuhakikisha haipotezi pesa hasa kwenye bima za afya na kwingineko.



# SHREE HINDUMANDAL HOSPITALI YENYE MIAKA 104

**Yaipongeza serikali Bima ya Afya kwa wote**

# SHREE HINDUMANDAL

## HOSPITALI YENYE MIAKA 104

MOJA kati ya Hospitali kongwe nchini ni Shree Hindu Mandal (SHM), iliyopo jijini Dar es Salaam.

MABADILIKO



**1931** Shree Hindu Mandal ilianzisha zahanati ya umma kama mtangulizi wa hospitali ya kisasa ya Shree Hindu Mandal yenye vitanda sitini hivi leo.



**Kwa sasa, hospitali inatoa huduma kwa wagonjwa wa nje kwa saa 24 ikijumuisha wodi ya dharura, majeruhi, kitengo cha wagonjwa mahututi**

DKT. KAUSHIKI RAMAIYA

MOJA kati ya Hospitali kongwe nchini ni Shree Hindu Mandal (SHM), iliyopo jijini Dar es Salaam. Hospital hii ilianzishwa Juni 29, 1919, chini ya Jumuiya ya Kihindi, dhamira yake kuu ikilenga kuwahudumia watu wa jamii hiyo.

### MALENGO

Kwa mujibu wa mkurugenzi wa Hospitali hii Dkt. Kaushiki Ramaiya alisema taasisi hiyo mbali ya kuanzishwa kwa ajili ya jamii ya Kihindu, pia iliundwa ikiwa na malengo na malengo makuu matatu kma yafuatayo:-

**01** Kukuza huduma za kijamii, kitamaduni, kidini, elimu na afya ya Jumuiya ya Wahindu na watu wa Tanzania bila kujali tabaka, rangi na imani.

**02** Kufanya, kukuza na kuendeleza shughuli za hisani na za kibinadamu.

**03** Kukuza na kuendeleza maelewano na mahusiano bora kati ya makundi mbalimbali ya watu wa Tanzania.

### MABADILIKO

Mnamo mwaka 1931, Shree Hindu Mandal ilianzisha zahanati ya umma kama mtangulizi wa hospitali ya kisasa ya Shree Hindu Mandal yenye vitanda sitini hivi leo.

### HUDUMA ZA SASA

Kwa sasa, hospitali inatoa huduma kwa wagonjwa wa nje kwa saa 24 ikijumuisha wodi ya dharura, majeruhi, kitengo cha wagonjwa mahututi chenye vitanda sita, radiolojia, maabara na duka la dawa.

Huduma za wagonjwa wa kulazwa kwa vitanda sitini huhudumia uzazi, matibabu, upasuaji, watoto na utaalamu mwingine.

Hivi karibuni hospitali hiyo imeongeza huduma za kusafisha damu na vitengo maalum vya VVU, Hepatitis B na hepatitis C pamoja na kitengo cha magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Hospitali pia inatoa huduma za kina za uchunguzi wa macho, huduma za tiba ya mwili na ina huduma maalum za VVU/ UKIMWI, TB na kisukari.

Hivi sasa hospitali hiyo inahudumia zaidi ya wagonjwa 500 wa nje kwa siku, ambao wanahudumiwa na jumla ya wafanyakazi 381 wakiwemo washauri, wataalamu, madaktari wakazi na wauguzi wenye utaalamu wa kina.

### BIMA YA AFYA KWA WOTE

Suala la bima ya afya kwa wote limepewa kipaumbele kikubwa na uongozi wa Hospitali hii na kwamba wanaamini ujio wa mpango wa bima ya afya kwa wote utakuwa na faida nyingi kuliko hasara.

**Hivi karibuni hospitali hiyo imeongeza huduma za kusafisha damu na vitengo maalum vya VVU**

# VISION Plus

kinara wa matibabu ya macho Tanzania

**Bima ya Afya ni muhimu kwa maendeleo ya taifa**

Tuna vifaa vya hali ya juu vya kutambua hali ya macho na kwenda na wakati tumewekeza katika teknolojia ya kisasa.

TOKAI
VISION PLUS ZANZIBAR

AFYA HOUSE OPP CLOUDS RADIO COCA COLA ROAD
ZANZIBAR TUPO MLANDEGE,BOMBAY BAZAAR,
TEL: 0778 227 252








**Viwango vya maambukizi ya upofu vinatofautiana sana lakini ushahidi unaonyesha kuwa upofu unazidi Afrika na Tanzania pia.**



# VISION Plus

kinara wa matibabu ya macho Tanzania

Kusema ukweli katika miaka 40 iliyopita tumejenga wateja wetu na lengo letu limekuwa kumtumikia kila mteja kutoka tabaka la chini hadi watu wa juu kabisa.





Mimi ni mtaalamu wa macho na kazi yangu ni kutoa huduma inayoeza kumsaidia mtu kuona,



Jarida la Tz&Beyond limefanya mahojiano na Daktari bingwa wa macho nchini Tanzania, ambaye pia ni mmiliki wa kituo bora cha kutoa huduma za macho cha Vision Plus, Dkt. Husseinali Datoo.

Dkt. Datoo ni mtu anayejulikana, amelitumikia taifa la Tanzania kwa huduma ya macho kwa zaidi ya miaka 40 sasa.

Huseinali Datoo alizaliwa Tunduru mkoa wa Ruvuma, ambapo wazazi wake waliishi huko na kufanya biashara tangu mwaka 1919.

Baada ya kumaliza masomo ya Sekondari kwenye shule ya Lindi alikwenda Uingereza na kusomea masuala ya Optometrist, alihitimu mwaka 1976 na kufanya kazi nchini humo kwa miwili kwenye mji wa London. Mwaka 1978 alirudi Tanzania.

**TZ&BEYOND:** Dkt. Datoo anafanya nini kwa sasa?
**DKT. DATOO:** Mimi ni mtaalamu wa macho na kazi yangu ni kutoa huduma inayoeza kumsaidia mtu kuona,



# VISION Plus

kinara wa matibabu ya macho Tanzania



tunaangalia macho na kupimia vipimo vya kuona na pia kufuatilia hali za macho zinazohusiana na matibabu na magonjwa kama vile kisukari, kudhibiti na kutibu shida ya Jicho Pevu na glakoma. Na pia tunatoa miwani.

**TZ&BEYOND:** Vision Plus imeanza lini?
**DK. DATOO:** Vision Plus awali ilijulikana kwa jina ya Medical Eye Centre ilianzishwa mwaka 1979. Tukiwa na kitengo kidogo kwenye barabara ya Morogoro jijini Dar es Salaam.

Baadaye tulipanuka hadi Zanzibar mwaka 1984 na maeneo mengine. Hapa Dar es Salaam tupo Shoppers plaza, Samora Tower na Afya house Mikocheni.

**TZ&BEYOND:** Kuna changamoto ya wataalamu wa macho, hapa hali ikoje?
**DK.DATOO:** NI dhahiri bado hatuna wahudumu wa afya wa macho wa kutosha kusaidia mamilioni ya watu wanaougua ugonjwa wa macho nchini.Hata hivyo jitihada zinaendelea na Wizara ya Afya za kutoa mafunzo na kuwawezesha wengi zaidi kusomea fani ya macho. Mwaka 1978 shule ya macho ilianzishwa mjini Moshi na tangu wakati huo imeanza nyingine Dodoma na Iringa hivyo katika miaka ijayo Tanzania itakuwa na wataalamu wengi wa macho natumai, hapa kwetu tunajitahidi, maana tunao wataalamu wa kutosha.

**TZ&BEYOND:** Suala la uhaba wa vifaa tiba vya macho nalo likoje?
**DK. DATOO:** Tuna vifaa vya hali ya juu vya kutambua hali ya macho na kwenda na wakati tumewekeza katika teknolojia ya kisasa.

Tuna kamera ambayo iligundua magonjwa kama vile kisukari,glaucoma ( shinikizo la macho). Pia tunaweke lenzi katika miwani na tunatumia mashine za kisasa.

**Vision Plus awali ilijulikana kwa jina ya Medical Eye Centre ilianzishwa mwaka 1979.**

**TZ&BEYOND:** Vision Plus inahudumia watu wa namna gani?
**DK. DATOO:** Kusema ukweli katika miaka 40 iliyopita tumejenga wateja wetu na lengo letu limekuwa kumtumikia kila mteja kutoka tabaka la chini hadi watu wa juu kabisa.

Itoshe kusema kwamba wateja wa hali ya juu wamekuwa nasi tangu kuanzishwa kwetu na huduma za macho tunazotoa ni za viwango vya juu.

**TZ&BEYOND:** Tatizo la macho ni kubwa kisi gani nchini?
**DK. DATOO:** Hivi majuzi tumeona matatizo mengi ya macho yanayohusiana na ugonjwa wa kisukari pamoja na hayo katika zama za matumizi ya simu janja, kompyuta pia husababisha tatizo la uoni hafifu kuongezeka nchini Tanzania.












**NI dhahiri bado hatuna wahudumu wa afya wa macho wa kutosha kusaidia mamilioni ya watu wanaougua ugonjwa wa macho nchini**



katika miaka 40 iliyopita tumejenga wateja wetu na lengo letu limekuwa kumtumikia kila mteja kutoka tabaka la chini hadi watu wa juu kabisa.







# VISION Plus

kinara wa matibabuya macho Tanzania

**Hali za kawaida za macho zinazosababisha kupoteza uwezo wa kuona au upofu ni: Mtoto wa jicho.¦Cataract¦ Retinopathy inayohusiana na ugonjwa wa sukari. Glakoma.¦shinikizo la damu la macho¦. Pia upungufu wa lishe ¦Vitamins¦ kwa Watoto wachanga.**

Hivyo nikiri, tatizo ni kubwa sana.

**TZ&BEYOND:** Mna mpango wa kufungua matawi zaidi?

**DK. DATOO:** Ndio, kama nilivyosema awali, tunayo matawi Dar es Salaam, lakini pia tunafikiria kufungua tawi Dodoma.

**TZ&BEYOND:** Hapa gharama za matibabu zikoje?

**DK. DATOO:** Ni kweli gharama za matibabu ya macho ni kubwa, lakini pia inategemea na tatizo linalomkabili mgonjwa.

Kwetu gharama ni za kawaida, siwezi kusema ni kubwa au ni ndogo.

**TZ&BEYOND:** Kipi ni kisababishi hasa cha matatizo ya macho?

**DKT. DATOO:** Viwango vya maambukizi ya upofu vinatofautiana sana lakini ushahidi unaonyesha kuwa upofu unazidi Afrika na Tanzania pia.

Chanzo kikuu ni pamoja na ujio wa kompyuta na simu na macho kupata uchovu kwa urahisi na kusababisha matatizo.

Hali nne za kawaida za macho zinazosababisha kupoteza uwezo wa kuona au upofu ni: Mtoto wa jicho. (Cataract) Retinopathy inayohusiana na ugonjwa wa sukari. Glakoma. (shinikizo la damu la macho).Pia upungufu wa lishe (Vitamins) kwa Watoto wachanga.

**TZ&BEYOND:** Nini kifanyike kulinda afya ya macho?

**DK. DATOO:** Kuna magonjwa mbalimbali ya macho na matatizo ya kuona. Baadhi yao hayana tiba, lakini wengine wengi wanaweza kutibiwa. Unaweza kujiepusha kwa kufuata mtindo mzuri wa maisha na kuangalia afya ya macho mara kwa mara.

**TZ&BEYOND:** Ushirikiano wa Vison Plus na Serikali ukoje?

**DK. DATOO:** Mimi binafsi, nimejihusisha na chama chetu cha wataalamu wa macho Tanzania Optometric Association (TOA) kwa miaka 20 sasa, nilikuwa sehemu ya mchakato wa juu wa kuhamasisha wadau kuanzisha Optometrist ACT 2017 Bungeni ambapo optometry ilitambulika kama taaluma nchini Tanzania.

Aidha, pia nimekuwa katika bodi ya Baraza la Optometria, niliteuliwa na Waziri ya Afya. Ambapo tunahakikisha kwamba Optometrists wanadhibitiwa kama taaluma zingine.

**TZ&BEYOND:** Ushiriki wa Vision Plus kwa jamii, ukoje?

**DKT.DATOO:** Tunaamini katika kurudisha kwa jamii yetu na uwajibikaji wa kijamii ndio dhamana kuu ambayo tumehusika nayo.

Tumekuwa tukifanya hivyo tangu 1984 na tumekuwa tukipanga kambi za macho kusaidia wasiojiweza.

Kambi ya macho ya kwanza ilikuwa Bagamoyo 1982 na baadaye Zanzibar mnamo 1985.

Kambi za macho zimekuwa zikiendelea na hadi leo tunashiriki na hayo.

Hapo Tunduru nilipozaliwa tulikuwa na kambi kubwa ya macho mwaka 2016 kwa kushirikiana na Bilal na tulihudumia watu wengi.

**TZ&BEYOND:** Matamanio yako ni yapo kwenye kukabiliana na tatizo la macho?

**DKT. DATOO:** Natamani kupanua zaidi uwajibikaji wetu wa kijamii wa shirika katika vijiji ambako kunahitajika huduma ya macho zaidi.



**Tunayo matawi Dar es Salaam, lakini pia tuna¦kiria kufungua tawi Dodoma.**








VISION Plus
kinara wa matibabu ya macho Tanzania


Chanzo kikuu cha ugonjwa wa macho ni pamoja na ujio wa kompyuta na simu na macho kupata uchovu kwa urahisi na kusababisha matatizo.



Ni kweli gharama za matibabu ya macho ni kubwa, lakini pia inategemea na tatizo linalomkabili mgonjwa

Kwetu gharama ni za kawaida, siwezi kusema ni kubwa au ni ndogo.








# TIPER

TANZANIA INTERNATIONAL PETROLEUM RESERVES L.T.D




TIPER BULK STORAGE







**TIPER** the joint venture company between the government of Tanzania and Oryx Energies SA (OESA) based in Geneva with equal shares 50% each operates the largest storage facility for petroleum in the country. Current storage capacity is 253.7 million litres.

TIPER which used to be known as Tanzanian Italian Petroleum Refining (TIPER) Company Limited, commissioned refinery business in 1966. In year 2000, the refinery business ceased. In 1999 Agippetrol International (BV) - "Agip" sold its assets in TIPER as well as the 50% shareholding of the company to Oryx Energies SA., GENEVA (OESA). The remaining 50% shares continued to be owned by the Government of Tanzania.

Following the liberalization of the downstream petroleum subsector in Tanzania, TIPER found it uneconomical to operate as a refinery. In mid-2000, the company changed its main objective from refining to petroleum product storage. The refinery was decommissioned, scrapped and the plant was then converted in to a refined petroleum storage terminal, whose core business is the bulk storage and handling of refined petroleum products with delivery of the customer's product through cross pumping to other terminals, back-loading for onward transshipment and truck loading for onward sale at local commercial and retail outlets as well as for transit.




**TIPER** operating as a bulk liquid storage entity, stores low sulphur diesel (AGO), Premium Motor Spirit " (PMS), Dual Purpose Kerosene (DPK) and Heavy Fuel Oil (HFO 180) which is widely used in industrial applications. TIPER operating as storage facility has facilitated to a greater extent the availability of petroleum products in the country as well as for neighboring land locked countries.

## TIPER'S CURRENT STORAGE CAPACITY BY PRODUCT IS SHOWN BELOW:

| Product | Capacity (Litres) |
|---|---|
| Diesel (AGO) | 180,246,000 |
| Premium Motor Spirit " (PMS) | 56,302,000 |
| Dual Purpose Kerosene (DPK) | 5,723,000 |
| HFO 180 | 11,383,000 |
| Total Storage Capacity | 253,654,000 |



# TIPER's *future* plan include:



To increase the capacity by adding more tankage to facilitate the envisaged opera tions of a special bonded warehouse and eventual Strategic Petroleum Reserve (SPR).

Lifting the operating standards in all fronts especially the HSSEQ and attain the ISO certification.

To gain validation in practical terms, to become the hub for petroleum supply chain for East and Southern Africa.

Enhancing Truck Loading Operations to facilitate operational efficiency for Various customers.










# Q&A

MAHOJIANO YA MWENYEKITI WA CHAMA CHA VITUO BINAFSI VYA AFYA NCHINI-ASSOCIATION OF PRIVATE HEALTH FACILITIES IN TANZANIA (APHFTA),

DKT EGINA FRANCIS MAKWABE.

## APHFTA:

# TUMEDHAMIRIA KUTOA HUDUMA BORA ZA AFYA NCHINI

**Tunatamani kukutana na Rais, tunayo mengi ya kuzungumza, nia yetu ni kutaka kuendelea kuwahudumia Watanzania na kuhakikisha mchakato wa Bima ya Afya kwa wote unakuwa na tija**

DKT EGINA FRANCIS MAKWABE.

DKT MAKWABE.

**TANGU kuruhusiwa kwa huduma ya afya kwa sekta binafsi, kumekuwa na mabadiliko makubwa yakiambatana na maboresho ya miundo mbinu, wataalam na vifaa tiba kwenye eneo hilo.**

**Hakuna shaka yoyote kuwa sekta binafsi imekuwa na mchango mkubwa kwenye eneo la huduma za afya. Sekta binafsi ndio ilikuwa ya kwanza kuleta mashine na vifaa mbalimbali vya upimaji wa magonjwa mbalimbali.**

Katika kulichambua hilo, jarida hili lilifanya mahojiano ya ana kwa ana na Mwenyekiti wa chama cha vituo binafsi vya afya nchini-Association of Private Health Facilities in Tanzania (APHFTA), Dkt Egina Francis Makwabe.

Dkt. Makwabe anaieleza APHFTA kuwa inajulikana kama Chama cha Vituo Binafsi vya Afya Tanzania, chama hiki kinajumuisha watoa huduma binafsi wote nchini.

Mbali ya kuwa Mwenyekiti wa APHFTA, Dkt. Makwabe pia ni mtaalamu wa magonjwa ya ndani ya mwili na ni Daktari bingwa wa ¦go.

**TZ¦BEYOND:** APHFTA imeanza lini na ina wanachama wangapi hadi sasa?

**DKT. MAKWABE**: APHFTA ilianza mwaka 1995¦96 miaka michache baada ya serikali kuridhia sekta binafsi kushiriki kwenye kutoa huduma kwenye eneo la afya.

Mpaka sasa hivi tuna wanachama zaidi ya 20,000 hapa ukijumlisha hospitali 1600, Zahanati na vituo vya afya binafsi nchi nzima zaidi ya 1000, maabara zinazojisimamia zaidi ya 1000, maduka ya dawa zaidi ya 1000 na maduka ya dawa baridi zaidi ya 18,000 nchi nzima.

**TZ¦BEYOND:** Unaweza kuzitaja kwa uchache hospitali ambazo zinaunda APHFTA?

**DKT. MAKWABE:** Baadhi ya wanachama wetu ni TMJ, Hindumandal, Aghakhan, Seife, Regency, Rabininsia, Kitengule, Kairuki na hospitali nyengine nyingi zilizopo kwenye mikoa yote nchini na mimi ndie Mwenyekiti wao, wameniamini niwaongoze.

**TZ¦BEYOND:** Majukumu ya APHFTA ni yapi?

**DKT. MAKWABE:** Majukumu yetu ni kuunganisha nguvu ya pamoja kwa Hospitali zote binafsi nchini, tunatambua kuwa Wizara ya Afya ndio mamwvuli na mlezi wa sekta nzima ya afya kwa upande wa serikali, lakini sisi tumeiona haja ya kuwa na kitu kinachotuunganisha ili linapokuja suala la kusema, wote tuwe na kauli moja, lakini pia tumeiona haja ya kuwa pamoja ili tutoe huduma bora za afya kwa watanzania wote.

Kwa sasa ndio tunachukua nafasi kubwa ya kutoa huduma ya afya kwa watu wengi nchini, ambapo kwa Dar es Salaam pekee yenye watu zaidi ya milioni tano, tunawahudumia asilimia 80¦ ya watu hao na asilimia 20 iliyobaki inahudumiwa na Serikali.

**TZ¦BEYOND:** APHFTA inakabiliwa na changamoto gani?

**DK.MAKWABE:** Changamoto kubwa ni kupungua kwa mapato, hii imesababishwa na vipindi tunavyopitia hasa Covid19 na Vita vya Ukraine na Urusi.

Mambo haya yametuteteresha sana, kumbuka tulilazimika kushiriki kikamilifu kwenye mapambano ya Covid 19, tumetumia rasilimali zetu nyingi katika kuwasaidia watanzania.

Kwa kiwango kikubwa kutetereka kwa uchumi wetu kumesababisha kushindwa kununua vifaa vikubwa zaidi vya kitabibu , kuajiri wataalamu zaidi, kutoa mafunzo kwa wataalamu tulio nao na kushindwa kuboresha miundo mbinu mipya.

Lakini pia tunakabiliwa na kodi, kama unavyofahamu sisi ni watoa huduma ambazo kwa muda mrefu tumekuwa tukihudumia watu wengi, tunalipa VAT na kodi nyingine, tunalipa tozo mbalimbali kama za OSHA na Fire, kwakweli tozo ni nyingi, ukiziorodhesha zote kodi na tozo kwa ujumla zinafika asilimia 52. Hiki ni kikwazo kwetu.

**TZ&BEYOND:** Unadhani kuna kodi na tozo zinapaswa kuondolewa?

**DKT. MAKWABE:** Ndio zipo, kwenye Blue Print ambayo ilikuwa ikisimamiwa na Waziri Mkuu walipendekeza kupunguza baadhi ya mambo hasa kwenye eneo la usimamizi na udhibiti na maeneo mengine waliyaunganisha ili kiwe kitu kimoja.

Kwa mfano kuna kanuni moja ya maabara inaitwa PHLD hii iliunganishwa na ile inayosajili hospitali, kimsingi zote zilikuwa zinafanya kazi zinazofanana, ila walijitofautisha kwenye vigezo ili kujipa uhalali, lakini kimsingi ni kitu kimoja.

Tulishiriki kuzisemea hizi na hatimae zikaunganishwa na kutupa ahueni, hatua hii ilikuwa ni mafanikio kwetu.

Changamoto nyengine ni kwamba huwezi kufugua Hospitali mpaka kila kitu kiwe kimekamilika, kwenye kufungua hospitali usajili huwa unachelewa sana huku tayari ukiwa umeshaajiri wafanyakazi na unawalipa mshahara, unatakiwa ufunge vifaa ambavyo havitumiki na pengine unakuwa umekopa na unatakiwa kurejesha mkopo na huku vibali vimechelewa.

**TZ&BEYOND:** Mlishawahi kukaa meza moja na serikali kuyazungumza haya?

**DKT. MAKWABE:** Hatujawahi kupata nafasi ya kukaa na Serikali kulieleza hilo, hatujawahi kupata jukwaa maalumu la kuyaongelea haya mambo ya kodi, lakini tunatamani hilo na matamanio yetu makubwa ni kupata nafasi ya kukutana na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan.

Huyu kiongozi ni msikivu na mwenye nia njema kwa sekta binafsi, tunatamani tupate nafasi ya kukaa nae mezani maana tuna mengi ya kuzungumza nae.

# Q&A



**APHFTA ilianza mwaka 1995/96 miaka michache baada ya serikali kuridhia sekta binafsi kushiriki kwenye kutoa huduma kwenye eneo la afya. Mpaka sasa hivi tuna**

DKT EGINA FRANCIS MAKWABE.

Lengo letu sisi si kuchangoea mtu au taasisi fulani, hapana, lengo ni kuitaka sekta hii binafsi indelee. Nadhani Serikali inatuhitaji na sisi tunaihitaji kwahiyo kama tungeweza kupata mazingira ambayo ni mazuri kwa utendaji ikiwemo kupatikana kwa usajili wa haraka ili tuweze kufanya kazi kwa haraka itasaidia sana maana tunaweka hela nyingi halafu hakuna thamani tunayopewa hasa na baadhi ya taasisi za serikali.

Imani yetu ni kwamba kama tutapata nafasi ya kuzungumza na rais inaweza kutusaidia kulainisha baadhi ya mambo ikiwa ni pamoja na kupata mikopo au hata ruzuku ukizingatia sekta binafsi tunajitolea sana katika kutoa huduma.

Mfano mzuri ni wakati wa COVID 19, watu walilazwa kwenye hospitali zetu walitumia Ventilators na vifaa vingine bure kabisa, pia tulishirikiana kutoa vifaa mbalimbali. Serikali ione haja ya kutenga angalau fungu kwa ajili ya kuboresha sekta binafsi, inaweza isiwe ruzuku ya bure, badala yake inaweza kuwa mkopo wenye riba nafuu, lengo ni kuboresha huduma za afya nchini.

**TZ&BEYOND:** Huduma nyingi bora ni kama mnazitoa mjini zaidi, vipi kwa maeneo ya vijijini?
**DKT. MAKWABE:** Wanachama wetu wanatumia mikopo kufanya shughuli zao, kwahiyo ni lazima uwekeze sehemu ambazo zina uhakika wa kurudisha ile pesa, ukiweka sehemu ambayo hutaweza kupata fedha ya kulipa mkopo ni wazi utauziwa nyumba zako zote na kila kitu, utafilisika. Kwahiyo mijini kote ndio APHFTA tupo kwasababu ndio sehemu unaweza ukaweka pesa na ikarudi, tumejikita kwenye miji mikubwa yote na makao makuu ya wilaya, vijijini tupo lakini ni kwa uchache.

**TZ&BEYOND:** Waeleze Watanzania umuhimu wa APHFTA kwenye sekta ya afya nchini.
**DKT. MAKWABE:** Kama nilivyosema awali chama hiki kimeunganisha watoa huduma wa afya binafsi wote na lengo ni kuwa na lugha moja. Lakini pia wanachama wetu wanatoa huduma bora za afya na tumekuwa tukishirikiana na serikali kwa urahisi maana lolote likitokea kwa mwanachama wetu sisi tunasimama pamoja kushughulikia suala hilo.



APHFTA:

# TUMEDHAMIRIA KUTOA HUDUMA BORA ZA AFYA NCHINI

**COVID 19, watu walilazwa kwenye hospitali zetu walitumia Ventilators na vifaa vingine bure kabisa, pia tulishirikiana kutoa vifaa mbalimbali.**

Umuhimu wetu ni mkubwa maana mbali ya kutoa huduma kwa asilimia 80, lakini pia tunatoa ajira kwa watanzania wengi, unajua kwa sasa wataalamu wa afya ni wengi na kila mwaka wanapatikana wapya ambao ni zaidi ya 1000, sasa kama kusingekuwa na hospitali binafsi maana yake hawa jamaa wangeenda wapi.

Aidha tunalipa kodi nyingi, hii inamaanisha tunachangia kwenye mfuko mkubwa wa serikali.

**TZ&BEYOND:** Nafasi ya kisheria ya APHFTA katika kushiriki kwenye maamuzi makubwa ya kisekta ikoje?
**DKT. MAKWABE:** Hakuna. Ni kweli tunafanya kazi pamoja na serikali, lakini kusema kweli hakuna sheria maalumu zinazoitambua sekta binafsi ya afya hasa katika kushirikishwa kwenye masuala ya kisheria, sisi tumepewa msimamizi ambaye anasimamia vituo vya afya kazi yake ni kusajili na kukagua tu, hajui tunachangamoto gani na wala tunataka nini. Kutokuwa na nafasi hiyo kisheria kunaleta shida kidogo, lazima kuwepo na sheria ambazo zingeiongoza sekta binafsi ishirikishwe kwenye mambo ya msingi ya kisekta.

Mfano mzuri ni suala la Bima ya Afya kwa Wote tumeshiriki, lakini ushiriki wetu ulikuwa ni kama wa waalikwa wengine tu, mipango yote na kila kitu kinafanywa na Wizara na sisi hatukushiriki kabisa kwenye maamuzi tangu mwanzo.
Kwahiyo kama ingekuwepo nafasi hiyo basi mambo yangekuwa mazuri zaidi kwakua tungeweza kuweka michango yetu ya msingi ambayo ingesaidia zaidi.





**Wanachama wetu wanatoa huduma bora za afya na tumekuwa tukishirikiana na serikali kwa urahisi maana lolote likitokea kwa mwanachama wetu sisi tunasimama pamoja kushughulikia suala hilo.**

DKT EGINA FRANCIS MAKWABE.









**Hitaji letu ni ushirikiano zaidi, kwa mfano wenzetu wa upande wa pili (Zanzibar) Mheshimiwa Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi ambaye ni Daktari wa binadamu, ameanza huo mfumo wa kushirikiana na sekta ya afya binafsi kwa kuwapa nafasi wawekezaji binafsi kujenga maabara karibu na hospitali.**



Utakumbuka mashine ya CT Scan ya kwanza katika nchi hii imekuja Hospitali ya Kairuki Mikocheni, kwahiyo tumekuwa ni watu ambao tunavumbua teknolojia mpya zaidi,



**Nikiwa Mwenyekiti wa APHFTA nasema tunaunga mkono bima ya afya kwa wote kwa sababu ni nzuri, ndio njia sahihi, itawapa nafasi watanzania kuzifikia huduma za afya kwa urahisi zaidi na kwa gharama nafuu.**

Nikiwa Mwenyekiti wa APHFTA nasema tunaunga mkono bima ya afya kwa wote kwa sababu ni nzuri, ndio njia sahihi, itawapa nafasi watanzania kuzifikia huduma za afya kwa urahisi zaidi na kwa gharama nafuu.

Niseme tu hatuna mgongano wa maslahi na Serikali na ndio maana ninasema tunafanya kazi kwa pamoja. Tunaushirikiano mzuri kabisa na lengo letu ni kutoa huduma bora za afya kwakufikia watu wengi na kila mahali nchini. Hitaji letu ni ushirikiano zaidi, kwa mfano wenzetu wa upande wa pili (Zanzibar) Mheshimiwa Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi ambaye ni Daktari wa binadamu, ameanza huo mfumo wa kushirikiana na sekta ya afya binafsi kwa kuwapa nafasi wawekezaji binafsi kujenga maabara karibu na hospitali.

**TZ& BEYOND:** Je, Bima ya Afya kwa Wote itafanikiwa?

**DKT. MAKWABE:** Itafanikiwa, lakini inatakiwa iwepo bima ambayo kila mtu atachangia na kwa wale ambao hawataweza kuchangia Serikali iwasaidie ambapo inatengwa kwenye bajeti. Lakini ili hili lifanikiwe ni lazima kuwe na njia sahihi ya kupata hizo fedha kutoka katika chanzo chochote ambacho Serikali itaamua ili kupata fedha kwa ajili ya kusaidia bima ya afya kwasababu matibabu ni gharama na usipofanya hivyo vituo vingi vya serikali vitashindwa kujiendesha. Kikubwa kuwe na fedha za kutosha ambazo zitaendana na kuongezeka kwa vituo vya kutolea huduma, kuwe na dawa za kutosha, madaktari, manesi, wauguzi, wafamasia wa kutosha na mengineyo ambayo yataendana na mahitaji yaliyopo kwa maana ya kutosha kuwahudumia watu.

**TZ&BEYOND:** Mafanikio ya APHFTA kwa ujumla ni yapi?



**Umuhimu wetu ni mkubwa maana mbali ya kutoa huduma kwa asilimia 80, lakini pia tunatoa ajira kwa watanzania wengi**

**DKT. MAKWABE:** Tangu tumeanza kazi tuna miaka zaidi ya 20 sasa na mafaniko makubwa ambayo sisi tunajivunia, moja ni kule kukubalika, tumekuwa tukifanya kazi na serikali kwa karibu sana, mawasiliano yamekuwa mazuri na tunaendelea kuboresha huduma kila siku, na tunafanya kazi na mashirika ya kimataifa kama vile DANIDA na USAID ambao wamekuwa wakitusaidia kwa upande wa msaada wa kitaalamu na ufadhili wa pesa kidogo, yote hiyo ni katika kuboresha huduma katika vituo vyetu.

Pili ni kuweza kutoa huduma za ubora wa hali ya juu kabisa, utakumbuka mashine ya CT Scan ya kwanza katika nchi hii imekuja Hospitali ya Kairuki Mikocheni, kwahiyo tumekuwa ni watu ambao tunavumbua teknolojia mpya zaidi, huduma za kusafisha damu na huduma za upasuaji kwa njia ya matobo zote zimefanyika nchini kwa mara ya kwanza kwenye hospitali binafsi na hii yote ni kwasababu tumeshikamana kama kitu kimoja.

Pia kama APHFTA tunatarajia mwaka huu kufanya mkutano mkubwa wa masuala ya afya ambao utahusisha nchi za Uganda, Burundi, Ethiopia, Kenya, Sudan Kusini, Rwanda na wenyeji Tanzania, tutakutana pamoja na kujadili masuala ya afya. APHFTA ni nguvu ya kuendesha mambo, ni chombo kikubwa ambacho kinavileta pamoja vituo vya afya vya binafsi, watengenezaji wa dawa, vifaa tiba na vinginevyo.

**TZ&BEYOND:** Uwiano wa wanawake na wanaume ukoje kwenye uongozi wa APHFTA?

**DKT. MAKWABE:** Kwa upande wetu kama APHFTA tunawathamini sana wanawake, kwenye uongozi wetu tunao wanawake na mmoja wao ni Katibu Msaidizi yeye ni mwanamke anaitwa Mama Chhaya ambaye ni mkurugenzi wa Hospitali wa TMJ.

**TZ&BEYOND:** Mapendekezo yenu kwa serikali ni yapi?

**DKT. MAKWABE:** Serikali yetu tunaipenda chini ya Mama Samia, kwasababu anazipa kipaumbele sekta binafsi na zinashamiri ila tunaomba tu kuwepo na sheria ambazo zitaitambua moja kwa moja sekta binafsi kwenye masuala ya Afya.

Urasimu upunguzwe ikiwemo usajili wa vituo uharakishwe kuliko watu kukaa muda mrefu wakisubiri.

Serikali ikiwa inatenga fedha iweke na kwa ajili ya Sekta binafsi, kuwe na mikopo nafuu.

Kuwe na ushirikiano wa hali ya juu katika Serikali na Sekta Binafsi ili tuweze kuendelea kutoa huduma bora.







Serikali inatoa Sh. bilioni 20 kila mwezi kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa dawa, hadi kufikia Desemba 2022 upatikanaji wake ulikuwa kwa asilimia 67 kutoka asilimia 62 Agosti, mwaka jana.

KUTOKA KWA

# MHARIRI MTENDAJI

## BIMA YA AFYA KWA WOTE ITASAIDIA KUWA NA TAIFA IMARA

AFYA ni mtaji, nchi yoyote yenye wananchi wenye afya na siha njema, kamwe uchumi wake hauwezi kutetereka, tofauti na nchi yenye wananchi wasioishiwa magonjwa.

Nchi yenye wananchi wachovu na waliotepeteshwa na maradhi, haiwezi kupiga hatua kwa sababu inakosa nguvu kazi na rasilimali watu wa uhakika.

Na njia pekee ya kuwa nan chi yenye watu imara wasio tetereshwa na maradhi ni kuwapo kwa uhakika wa matibabu bora, ya haraka na yanayohimilika.

Sote tunatambua ughali wa gharama za matibabu, duniani kote. Matibabu si rahisi, gharama za matibabu hazijawahi kuwa ndogo na hasa kwa maradhi yasiyo ya kuambaukiza ambayo yanawasumbua zaidi vijana na wazee, ambao ndio nguvu kazi yenyewe.

Njia pekee ya kuondokana na maumivu ya gharama za matibabu zinatajwa kuwa ni Bima ya Afya na hili kiukweli halina ubishi.

Hata hivyo bado kuna changamoto kidogo kwa watu kutambua umuhimu wa bima ya afya, lakini pia gharama za kulipia huduma hiyo nazo zinatajwa kuwa kubwa.

Hali hiyo inawafanya wananchi wengi kujiweka kando na kufanya asilimia nane tu ya Watanzania ndio kuwa na uwezo wa kumiliki Bima ya afya na wengi wao wakiwa ni watumishi wa umma.

Kwa kulitambua hilo, serikali imeiona haja ya kuanzisha mchakato wa Bima ya Afya kwa wote. Hii maana yake ni kumpa kila mtanzania uhakika wa kutibiwa kama zinavyofanya baadhi ya nchi za nchi kama vile Rwanda, nchi za Scandnavia, Ghana, Norway, Finland na Japan

Hata hivyo mchakato huo bado haujakamilika, haujakamilika kwa sababu mswaada wa sheria ya suala hilo unakabiliwa na vikwazo kadhaa, ambavyo ni vya msingi.

Vikwazo hivyo vilisababisha mswaada huo kutoingizwa bungeni ili kujadiliwa na kupitishwa kama sheria ili ukasainiwe na rais na kuwa sheria kamili.

Tayari umeshakwama mara mbili na matarajio yaliyopo sasa ni kulitumia Bunge hili linaloendelea kuupitisha ili ujadiliwe na ikiwezekana uanze kutumika mwaka huu.

Sisi TZ&BEYOND tunaamini mswaada huo unastahili kuingizwa bungeni ili ujadiliwe na hatimae kuwa sheria.

Tunaliamini hilo kwa sababu ya hali halisi ilivyo kwa sasa kwenye gharama za matibabu. Kama tulivyotangulia kuandika hapo juu kuwa gharama za matibabu ni ghali na hilo linachangia watu wengi kushindwa kupata tiba sahihi ya maradhi yanayowasibu hatima yake ni baadhi yao kupoteza maisha na wengine kupata ulemavu wa kudumu kutokana na kukosa matibabu bora.

Kama ilivyo dhamira njema ya serikali ya awamu ya Sita ambayo inaongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, nasi tunajiona tunalojukumu la kuchochea na kuchagiza umuhimu wa kila mtanzania kuwa na uhakika wa Bima ya Afya.

Tunatambua suala hilo linahitaji maandalizi ya kutosha hasa katika kuhakikisha kunakuwa na mfumo mzuri na imara wa kupata fedha za kuwachangia wasio na uwezo, lakini pia kuhakikisha kila mwenye uwezo wa kuchangia anafanya hivyo.

Haliwezi kuwa suala jepesi, lakini ni vema kama nchi tukawa tayari kukabiliana na changamoto hizo kwa kadiri zitakavyojitokeza.

Rai yetu kwa Bunge, likubali kuuingiza mswaada huo ili ujadiliwe, tunajua dhamira ya Bunge ni njema, Bunge linataka kuhakikisha mchakato huo haukwami mara baada ya kuanza, lakini ili kuipa afya dhamira hiyo njema ni vema likashauri na kuhakikisha mambo yanakwenda na si kutoridhia kuujadili.

TZ&BEYOND tunaamini njia sahihi na bora za kukabiliana na changamoto hizo ni kushirikiana kwa karibu na wadau wa sekta ya afya bila kujali wanatoka upande upi, kama kuna haja ya kuwashirikisha tena wadau, washirikishwe wote wa sekta ya umma na binafsi. Hakuna jambo linaloharibika mbele ya wengi.

Chonde chonde Bunge letu, tunaomba muupe nafasi mswaada huo ili ujadiliwe na hatimae wananchi wapate kile wanachostahili kukipata.

Bunge letu ni sikivu na lenye dhamira ya kumtetea kivitendo mwananchi ambaye ndie mpiga kura. Sisi tunaamini mswaada huo wa Bima ya afya kwa wote utajadiliwa na utakapokuwa sheria utakuwa na tija kubwa kwa nchi na wananchi.

**Mungu Ibariki Tanzania...**



Jimmy C. Kiango
MHARIRI MTENDAJI



VISION PLUS EYE CLINIC

TIPER BULK STORAGE

TANZANIA REVENUE AUTHORITY
ISO 9001: 2008 Certified

TIB CORPORATE BANK
Your Partner Bank

KCB BANK

Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

CRDB BANK
Tunakusikiliza

NSSF
BOARD OF TRUSTEES NATIONAL SOCIAL SECURITY FUND

# SHUKRANI
za dhati kwa WASHIRIKA WETU




**Experience the power of TemboCARD**

Shop locally and internationally at over 44 million merchants and 2 million ATMs

VISA

CRDB BANK
The bank that listens